‘Ho-hum’ au Nahumu

Sura ya 9
Somo la Kusikiza: Agano la Kale Namba 82

Shabaha: Kuelewa utakatifu na upendo katika ujumbe wa Nahumu.

BWANA ni mwema, ni ngome siku ya taabu; naye huwajua hao wamkimbiliao, lakini kwa gharika ifurikayo atapakomesha kabisa mahali pake, na kuwafutia adui zake hata gizani.

- Nahumu 1:7-8

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Krsito Yesu Bwana wetu.

- Warumi 6:23

Washami waliwashinda na kuwafanya watumwa mataifa yote ya ulimwenguni kwa ukatili usioelezeka. Wanapofanyika milki kuu ya ulimwengu, ulimwengu kwa jumla uliogopa sana ukatili wao. Mji mkuu wa milki ya Washami ulikuwa mji wa Ninawi. Hata kama mji huu ulikuwa umetubu kutokana na mahubiri ya Yona, Washami walishinda kwa vita Ufalme wa Kaskazini wa Israeli yapata miaka 60 pekee baadaye. Baada ya miaka mingine 60 ya uvamizi huo, Washami walitishia Ufalme wa Kusini wa Yuda. Hapo ndipo nabii Nahumu alinena maneno ya faraja kwa Yuda: Kitambo kidogo, Ninawi mji mkuu wa maadui zao ungeenda kuharibiwa. Kwa sababu ya tabia yake takatifu na yenye haki, Mungu angekabiliana na Washami vikali na kuwaadhibu kwa dhambi zao za ukatili.

1. Ukweli au uongo? Sawa na Yona, Nahumu pia alihubiri ujumbe kuhusu Ninawi.

2. Ukweli au uongo? Kutubu kwa Ninawi wakati wa Yona kulidumu kwa karne nyingi.

3. Ukweli au uongo? Ninawi ndio uliokuwa mji mkubwa ulimwenguni wakati wa Nahumu.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

4. Linganisha sura tatu za Nahumu kila moja na mada inayolingana nayo:

a. Sura ya 1	i. Kushindwa kwa Ninawi kwazuiliwa
b. Sura ya 2	ii. Kushindwa kwa Ninawi kwatangazwa
c. Sura ya 3	iii. Kushindwa kwa Ninawi kwafafanuliwa

5. Ninawi ilichukuwa muda gani kuanguka baada ya unabii wa Nahumu?
   a. Majuma 2
   b. Miaka 3 na nusu
   c. Miaka 23
   d. Miaka 120

6. Nahumu aliishi wakati gani?
    a. Punde baada ya nabii Eliya
    b. Kabla ya umateka wa Babiloni, karibu na wakati wa Isaya
    c. Karibu na wakati wa Yesu
    d. Hatujui maelezo yoyote ya maisha yake

7. Vitabu vya kinabii mara nyingine vinajumuishwa kama ‘kuanguka kwa miji minne.’ Hizi miji ni gani? *(chagua miji zote sahihi)*
    a. Roma
    b. Yerusalemu
    c. Dameski
    d. Susa
    e. Atheni
    f. Ninawi
    g. Babiloni
    h. Gathi
    i. Samaria

8. Ujumbe wa Nahumu kwa watu wa Yuda ulikuwa upi?
    a. Hawatahitaji kuwa na wasiwasi kuhusu Ninawi kuwavamia tena
    b. Wataharibiwa pamoja na Ninawi
    c. Watakombolewa tu baada ya Ninawi kuwashikilia matekani kwa miaka 70
    d. Watachukuliwa mateka na kutawanywa na Ninawi kama ilivyokuwa na Ufalme wa Kaskazini

9. Kwa nini Mungu alimwaka ghadhabu yake juu ya Ninawi?
    a. Walikuwa wamefanyika watu wasiotubu na pia walikuwa wamefanya ukatili mbaya sana
    b. Walikuwa wanaendeleakua wenye nguvu zaidi kushinda Mungu kukabiliana nao
    c. Hawakuwa wa muhimu sawa na watu wengine
    d. Alitaka kuonyesha nguvu zake

10. Nahumu anasema nini kuhusu tabia ya Mungu?
    a. Mungu ni wa kupenda tu na hawezi kasirika
    b. Mungu ni wa kukasirika tu na hawezi onyesha upendo
    c. Mungu ni wa kupenda na mtakatifu, na hukasirishwa na dhambi
    d. Mungu hana haja na mambo ya wanadamu

11. Kwa nini kitabu cha Nahumu ni ujumbe muhimu kwetu leo?
    a. Kinatuonyesha kuwa Mungu huwapenda watu fulani pekee
    b. Kinatuonya tuombe ili maadui zetu waangamizwe kabisa
    c. Kinatabiri kuwa Ninawi itajengwa tena katika siku zetu ili ipigane na watu wa Mungu
    d. Ni somo la vile upendo wa Mungu unaonyeshwa kupitia hasira zake na hilo linatusaidia kuelewa kwa nini anachukia dhambi

Kwa nini Mungu anachukia dhambi? Ni vipi hasira zake dhidi ya dhambi zinaonyesha kuwa anatupenda? Je, kunaye rafiki au mtu wa familia ambaye hajakubali kipawa cha Mungu cha uzima wa milele? Unawezaje kushiriki upendo wa Mungu na wao?

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kuwa anakupenda sana mpaka hawezi puuza dhambi katika maisha yako. Muulize akufanye uwe hodari kinyume na majaribu, na uulize kuwa aweke hisia zake ndani ya moyo wako. Muulize Mungu akusaidie kushiriki ujumbe wake wa upendo na wote wanaouhitaji.

KUZAMA ZAIDI

1. Ni katika njia gani unabii wa Nahumu kuhusu uharibifu wa Ninawi ulikuwa habari njema kwa watu wa Mungu? _____
_____
_____
_____

2. Ukilinganisha kitabu cha Nahumu na kile cha Yona, ni mkataa gani unaolazimika kuufanya kuhusu wokovu usio wa kawaida wa Ninawi kupitia nabii Yona? _____
_____
_____
_____

3. Matumizi ya matendo ya kujitolea ya kitabu cha Nahumu kwa maisha yetu ni gani? _____
_____
_____
_____

4. Kwa njia gani Nahumu anazuia uharibifu wa Ninawi? _____
_____
_____
_____

5. Ukitafakari kwa makini ukatili mbaya muno wa Washami, je, kitabu hiki kinamaanisha kuwa Mungu atavumilia tu utawala mbaya na mwovu kwa kiwango fulani tu kisha ataufutilia mbali?
_____
_____
_____
_____

6. Ushinde wa Ninawi miaka 23 baada ya unabii huu kutangazwa, ulimthibitishaje Nahumu kama nabii? _____
_____
_____
_____

7. Nabii Nahumu alishukulikia kizuizi gani kilichokuwa kinazuia kazi ya Mungu? _____
_____
_____
_____